



**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA AFYA
TAARIFA KWA UMMA**

MWENENDO WA UGONJWA WA CORONA NCHINI TAREHE 22 APRIL, 2020

Wizara ya Afya, Zanzibar inatoa taarifa ya ongezeko la wagonjwa wapya tisa **(9)** wa Corona (COVID-19) Nchini na kufikia idadi ya wagonjwa themanini na tatu **(83)** kutoka sabini na nne **(74)** ambao tuliowatolea taarifa tarehe 20 Aprili 2020.


Wagonjwa hawa wote ni Raia wa Tanzania na wanaishi Unguja.

Serikali kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kuwasisitiza Wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwemo unawaji wa mikono kwa maji ya kutiririka na sabuni, kuepuka misongamano na kuahirisha safari za Nje na ndani ya Nchi zisizo za lazima. Tunawaagiza Wananchi wote kuvaa barakoa muda wote wanapotoka nje ya nyumba zao. Utaratibu wa uvaaji wa barakoa na aina gani ya barakoa utatolewa na Serikali.

Aidha Wizara inaomba Wananchi ambao wana dalili za homa kali, kukohowa na kupiga chafya kujitokeza katika vituo vyetu vya afya au kupiga simu namba 190. Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine na tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo vinavyo husiana na ugonjwa huo.

Pia vyombo vya habari vinahimizwa kupata taarifa za ugonjwa huu wa COVID-19 kutoka Wizara ya Afya.

Ndugu wananchi tuendeleo kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kutuepusha na maradhi haya.


Hamad Rashid Mohamed (MBM)(MBLW),
Waziri wa Afya - Zanzibar.